

*Mifugo kujenga vizimba 8 Geita kuzalisha samaki

**Na Yohana Shida,
Geita**

WAZARA ya Mifugo na Uvuvi imepanga kujenga vizimba vikubwa vinane vya kufugia samaki ndani ya Ziwa Victoria mkoani Geita ili kuongeza uzalishaji wa samaki kwa ajili ya biashara na chakula mkoani humo.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba

Ndaki ametoa taarifa hiyo juzi kwenye mkutano wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Alifafanua mradi huo ni matokeo ya utafiti wa mazingira uliofanyika ndani ya Ziwa Victoria kwenye maeneo ya mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Mara na Simiyu na kujiridhisha Geita ni miongoni mwa maeneo rafiki kwa mradi.

"Sasa hili ni eneo ambalo naomba wanchi wa Geita tuchan-

gamkie, maana ni eneo ambalo yeye aliye tayari ndio atapewa maeneo hayo ili afanye shughuli za ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba, tuweze kuuza samaki kwa wingi," alisema.

Aliongeza pia kuna ujenzi wa chuo kikubwa cha mafunzo ya ufugaji wa samaki na viumbe vya majini wilayani Chato ambapo ndani yake kutakuwa na mabwawa tisa pamoja na kituo cha kutotolesha vifaranga

vya samaki.

"Vijana kutoka maeneo ya kanda hii watakwenda kwenye eneo hilo watafundisha ili waweze kuzalisha samaki kwa wingi kwa njia ya ufugaji wa zamani," alisisitiza.

Alieleza hatua hiyo inalenga kutimiza azma kuu mbili ambazo ni kuongeza tija katika sekta za ufugaji na uvuvi na kuweka mazingira wezeshi kwa shughuli hizo ziweze kufanyika kibiashara zaidi.

Mo
taif
kuf
kuf
ura

we
tak
ka
ku

ge
zi
ya
isl
ki

m
su
k
k
n

k
k
l

y

s

o

o

Sh13.5 bil kusaidia ufugaji kuku nchini

Tuzo Mapunga, Mwananchi
tmapunda@Mwananchi.co.tz

Dar es Salaam. Ikiwa ni sehemu ya kusaidia ufugaji kuku wa kisasa na wenye tija, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) imetoa kiasi cha Sh13.5 bilioni kwa wafugaji wa kuku waliopo sehemu mbali mbali hapa nchini.

Hayo yalisemwa na Ofisa mwanadamizi wa maendeleo ya biashara wa TADB, Grayson Ferdinand wakati wa maonesho ya sita ya kuku na ndege wafugwao yaliyofanyika mwishoni mwa wiki jijini hapa.

Alisema sekta ya ufugaji kuku, ina mchango mkubwa katika kutengeneza ajira kwa makundi mbalimbali wakiwamo wanawake na vijana, na kuongeza kuwa benki hiyo itaendelea kutoa mikopo katika sekta hiyo na kusaidia ukuaji zaidi.

"TADB inawekeza kwenye sekta ya kuku, kwa sababu ya usalama wa chakula na pia sekta hii muhimu ni chanzo cha ajira kwa wanawake na vijana wengi. Lengo letu ni kuona sekta inatoa mchango zaidi na TADB itaendelea na kutoa mikopo kwenye sekta hii ili kuhakikisha pia wafugaji wengi zaidi wananufaika," alisema

Alitoa wito kwa wafugaji wa kuku nchini kuchangamkia fursa ya mikopo



'Maonyesho hayo ya siku mbili yaliwaleta pamoja wafugaji na wadau mbalimbali katika sekta ya ufugaji kuku ambao walionyesha bidhaa mbali mbali.

inayotolewa na benki hiyo, ili waweze kufanya upanuzi wa miradi yao na kuongeza uzalishaji na hatimye kufikia lengo la mahitaji katika sekta hiyo..

Sekta ya Kuku nchini imezidi kukua

kwa kasi huku ikikadiriwa kuwa na Kuku zaidi ya milioni 100 katika mashamba tofauti.

Pamoja na ukuaji huu mkubwa mahitaji ya kuku bado ni makubwa ukilinganisha na mahitaji ya Watanzania zaidi ya milioni 60. Maonyesho hayo ya siku mbili yaliwaleta pamoja wafugaji na wadau mbalimbali katika sekta ya ufugaji kuku ambao walionyesha bidhaa mbali mbali mbali zinatokana na kuku na pia kuwakutanisha kwa ajili ya kubadilishana uzoefu.